Australian Human Rights Commission

Kutoa malalamiko

Tume ya Haki za Binadamu ya Australia ni shirika linalojitegemea ambalo huchunguza na kutatua malalamishi kuhusu ubaguzi wa kijinsia, umbari, ulemavu na umri, ubaguzi wa ILO III na ukiukaji wa haki za binadamu.

Unachoweza kutulalamikia kuhusu

- ***Ubaguzi wa kijinsia*** ni pamoja na unyanyasaji na ubaguzi unaohusiana na jinsia, utambulisho wa jinsia, hali ya kuwa na jinsia mbili, ujauzito, hali ya ndoa au uhusiano, kunyonyesha, wajibu wa familia na maelekeo ya kingono.
- ***Ubaguzi wa ulemavu*** ni pamoja na ubaguzi unaohusiana na ulemavu wa kimwili, kiakili, kihisia, kujifunza na magonjwa ya kiakili; ugonjwa, hali za matibabu, jeraha zinazohusiana na kazi, ulemavu wa awali, wa sasa na wa baadaye; na kuhusishwa na mtu aliye na ulemavu.
- ***Ubaguzi wa kimbari*** ni pamoja na chuki ya kimbari na ubaguzi kutokana na umbari, rangi, ukoo, taifa au asili ya kabila na hali ya uhamiaji.
- ***Ubaguzi wa umri*** ni pamoja na ubaguzi kutokana na kuwa mdogo sana au mzee sana.
- ***Ubaguzi wa ILO III*** ni pamoja na ubaguzi wa dini, rekodi ya jinai, shughuli ya chama cha wafanyakazi, maoni ya kisiasa na asili ya jamii.
- ***Haki za binadamu*** inajumuisha vitendo na au kwa niaba ya Jumuiya ya madola ambavyo vinadaiwa kukiuka vyombo vya kitaifa vya haki za binadamu, kama vile Mapatano ya Kitaifa kuhusu Haki za Raia na Kisiasa, Mapatano kuhusu Haki za Mtoto na Mapatano ya Haki za Watu walio na Ulemavu.

Unaweza kufanya malalamiko bila kujali unapoishi Australia na haina gharama kufanya malalamiko. Hatua katika utendaji zimeelezewa kwa mhutasari hapa chini.

Uliza swali

- Ikiwa huna uhakika kama unaweza kutoa malalamiko kuhusu jambo, unaweza kuwasiliana na Huduma ya Maelezo ya Malalamishi ya Tume kwa simu kwenye **1300 656 419** au kwa barua pepe kwa complaintsinfo@humanrights.gov.au.
- Tunaweza kukutumia fomu ya malalamiko ili kuanza utendaji.
- Ikiwa hatuwezi kukusaidia, tutajaribu kukueleka kwa mtu ambaye anaweza.

Toa malalamiko

- Malalamiko lazima yaandikwe. Unaweza kujaza fomu ya malalamiko na ututumie kwa posta au uitume kwa pepesi au unaweza toa malalamiko yako mtandaoni kwenye tovuti wetu. (www.humanrights.gov.au)
- Unaweza kutoa malalamiko katika lugha yako unayopenda na tunaweza kukusaidia kuandika malalamiko yako ikiwa itahitajika.
- Huhitaji wakili ili kutoa malalamiko.
- Ikiwa hatuwezi kushughulikia malalamiko yako, tutaelezea kwa nini.

Uchunguzaji

- Tutawasiliana nawe ili kuzungumzia kuhusu malalamiko yako na tunaweza kukuuliza kutoa maelezo zaidi.
- Kwa kawaida, Tume itawasiliana na mtu au shirika unalolalamika, wape nakala ya malalamiko yako na uulize maoni yao na maelezo mengine husika. Tutakujulisha ambacho wamesema kuhusu malalamiko yako.
- Katika hali zingine tunaweza kuamua kutoendelea kushughulikia malalamiko yako. Ikiwa hii itatokea, tutaelezea kwa nini.
- Tunaweza kuzungumza nawe kuhusu kujaribu kutatua malalamiko kwa upatanisho.

Upatanisho

- Upatanisho unamaanisha ya kwamba tunajaribu kukusaidia wewe na mtu au shirika unalolalamika kuhusu kupata njia ya kutatua suala.
- Upatanisho unaweza kuwa mkutano wa uso kwa uso unaojulikana kama ‘mkutano wa upatanisho’ au kupitia mkutano wa simu. Katika hali zingine malalamiko yanaweza kutatuliwa kupitia ubadilishaji wa barua au kupitia ujumbe kwa simu au baruapepe kupitia mpatanishi.
- Malalamiko yanaweza kutatuliwa katika njia nyingi tofauti. Kwa mfano kwa msamaha, ubadilishaji wa sera au fidia.

Hatua ya mahakama inayowezekana – ubaguzi wa jinsia, ulemavu, mbari na umri

- Tume haina uwezo wa kuamua ikiwa ubaguzi kinyume cha sheria umetokea.
- Ikiwa malalamiko yako hayatatuliwa au hayataendelea kwa sababu nyingine, unaweza kupeleka suala mahakamani. Mahakama inaweza kuamua ikiwa ubaguzi kinyume cha sheria umetokea.
- Una siku 60 kutoka wakati Tume inakamilisha malalamiko ili kufanya ombi kwa Mahakama ya Mzunguko ya Shirikisho ya Australia au Mahakama ya Shirikisho ya Australia.
- Tume haiwezi kukupelekea suala mahakamani au kukusaidia kuwasilisha kesi yako mahakamani.
- Unaweza kuhitaji kuzungumza na wakili au huduma ya sheria ikiwa unataka kwenda mahakamani.

Uamuzi/Ripoti-ILO III ubaguzi na haki za binadamu

- Ikiwa malalamiko hayajasuluhishwa au kutoendelea kwa sababu nyingine, Rais wa Tume ataamua ikiwa ubaguzi wa ILO III au ukiukaji wa haki za binadamu umetokea. Hii inaweza kujumuisha Rais kufanya kikao cha umma ambapo kila upande unawakilisha toleo lao la matukio na anajibu maswali.
- Ikiwa Rais ametosheka ya kwamba ubaguzi au ukiukaji wa haki za binadamu ulitokea, Rais ataripoti suala kwa Mwanasheria Mkuu wa Shirikisho. Katika ripoti, Rais anaweza kupendekeza fidia ya hasara au jeraha lolote ambalo mtu amepata. Riporti lazima itolewe katika mbunge.
- Mifano ya uamuzi wa Rais kuhusu ubaguzi na haki za binadamu zinapatikana katika tovuti ya Tume http://www.humanrights.gov.au/publications/reports-minister-under-ahrc-act.

Naweza kupata wapi maelezo zaidi?

Maelezo ya anwani ya Tume ya Haki za Binadamu Australia ni:

Simu

Simu ya maelezo ya malalamiko:	1300 656 419 (simu ya ndani)
TTY:	1800 620 241
NRS:	133 677
Faksi:	(02) 9284 9611

Ikiwa unahitaji mfasili unaweza kupigia **131 450** na uulize kuunganishwa kwa Tume ya Australia ya Haki za Binadamu.

Ikiwa wewe ni kiziwi au una matatizo ya kusikia unaweza kuwasiliana nasi kwa TTY kwenye 1800 620 241. Ikiwa wewe una matatizo ya kusikia au kuzungumza unaweza pia kuwasiliana nasi kupitia National Relay Service (NRS) kwa 133 677. Ikiwa unahitaji mfasili wa Kiauslan, Tume inaweza kukupangia hii.

Ikiwa wewe ni kipofu au una shida ya kuona, Tume inaweza kutoa maelezo katika fomati mbadala kwa maombi.

Posta

Australian Human Rights Commission
GPO Box 5218
Sydney NSW 2001

Mtandao

Barua pepe:	complaintsinfo@humanrights.gov.au
Tovuti:	www.humanrights.gov.au

Unaweza kutoa malalamiko mtandaoni kwa kwenda kwa http://www.humanrights.gov.au/complaints/lodging-your-complaint.

Mawaidha ya kawaida ya kisheria

Ikiwa unafikiria kutoa malalamiko, pia unaweza kufikiria kupata mawaidha ya kisheria au kuwasiliana na shirika la jamii. Kuna huduma za `kisheria za jamii ambazo zinaweza kutoa mawaidha yasio ya malipo kuhusu ubaguzi na usumbufu. Maelezo ya mawasiliano ya kituo cha kisheria cha jamii cha karibu yanaweza kupatikana www.naclc.org.au/directory.

Kanusho: Maelezo kwenye karatasi hii yananuiwa tu kama mwongozo. Sio kibadala cha mawaidha ya kisheria.